## SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

### MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Marekebisho ya Sheria mbali mbali.


**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI NAM. 7 YA MWAKA 2018**


3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 2.

5. Kufuta na kuandika upya kifungu cha 151.


**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI NAM. 8 YA MWAKA 2015**


6. Kusomwa.

7. Marekebisho ya kifungu cha 2.

8. Marekebisho ya vifungu vya 3(1), 13(b), 13(c), 13(d), 14 (1)(b), 15(a), 19(7), 19(8), 25(1), 38(5), 38(6), 38(7), 38(8), 38(9), 46(1), 46(3)(b), 46(3)(i), 59(1) na 67.

9. Marekebisho ya kifungu cha 9.

10. Marekebisho ya kifungu cha 14(1).

11. Marekebisho ya kifungu cha 15.

12. Marekebisho ya kifungu cha 20.

13. Marekebisho ya kifungu cha 30.

14. Marekebisho ya kifungu cha 38.

15. Marekebisho ya kifungu cha 44.

16. Kuongeza Vifungu Vipya vya 44A, 44B na 44C.

**SHERIA NAM. 1 YA 2021**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

08. 03, 2021

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali, 2021 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika Sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoainishwa katika Sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI, NAM. 7 YA MWAKA 2018

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Nam. 7 ya Mwaka 2018, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**4.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 2 kwa kufuta maneno "... ambalo dhamana inaweza kutolewa na Jaji Mkuu tu chini ya kifungu cha 151(4) cha Sheria hii" yanayoonekana katika tafsiri ya maneno "kosa lisilo na dhamana".

Kufuta na kuandika upya kifungu cha 151.

**5.** Kifungu cha 151 cha Sheria Mama kinafutwa na kuandikwa upya kifungu cha 151 kama ifuatavyo:

Uwezo wa jumla wa kutoa dhamana.

**151.**-(1) Pale mtu yeyote, asiyekuwa mtu anayeshtakiwa kwa kuuwa kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume, kubaka kwa kikundi, kuingilia maharimu, kumnajisi mtu mwenye ugonjwa wa akili, utakatishaji wa fedha haramu, kukwepa kodi au matumizi mabaya ya mali, anakamatwa au anawekwa kizuizini bila ya hati ya ukamataji na mkuu wa kituo cha polisi, au anafika au analetwa mbele ya mahakama, na yupo tayari wakati wowote wakati yupo kwenye hifadhi ya afisa huyo au katika hatua yoyote ya mwenendo wa shauri mbele ya mahakama hiyo kuweka dhamana, mtu huyo anaweza kupewa dhamana.

(2) Mkuu wa kituo cha polisi au mahakama, badala ya kuchukuwa dhamana kutoka kwa mtu huyo, inaweza kumuachia mtu huyo atakapotekeleza ahadi ya dhamana bila ya wadhamini kwa ajili ya kuhudhuria kwake kama itakavyoelezwa baadae.

(3) Kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana.

(4) Mahakama Kuu inaweza, katika kesi ya makosa yenye dhamana, kuelekeza kwamba mtu yeyote apewe dhamana au kwamba masharti ya dhamana yaliyowekwa na mahakama ya chini au polisi yapunguzwe.

(5) Endapo mtu ameshindwa kutekeleza masharti ya ahadi ya dhamana kuhusu muda na pahala pa kuhudhuria, mahakama inaweza kukataa kumuachia mtu huyo kwa dhamana kwa mara nyengine baadae katika kesi hiyo ambapo atafika mbele ya mahakama au ataletwa kwenye kizuizi, na kukataa huko kokote kutakuwa bila ya kuathiri mamlaka ya mahakama kumuita mtu yeyote anayewajibika na ahadi hiyo kulipa adhabu inayotokana na ahadi hiyo.

(6) Ukiukaji wa ahadi ya dhamana ya polisi unaweza kutiliwa nguvu za kisheria mahakamani kwa kutumia masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, NAM. 8 YA MWAKA 2015

Kusomwa.

**6.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mashirikiano baina Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Nam. 8 ya mwaka 2015, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya neno "Waziri" popote linapoonekana katika kifungu cha 2 na kuweka badala yake tafsiri mpya ya neno "Waziri" kama ifuatavyo:

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya vifungu vya 3(1), 13(b), 13(c), 13(d), 14 (1)(b), 15(a), 19(7), 19(8), 25(1), 38(5), 38(6), 38(7), 38(8), 38(9), 46(1), 46(3)(b), 46(3)(i), 59(1) na 67.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno "Wizara ya Fedha" yanayoonekana katika vifungu vya 3(1), 13(b), 13(c), 13(d), 14 (1)(b), 15(a), 19(7), 19(8), 25(1), 38(5), 38(6), 38(7), 38(8), 38(9), 46(1), 46(3)(b), 46(3)(i), 59(1) na 67 na kuweka badala yake maneno "Wizara inayohusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**9.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno "... Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar" yanayoonekana katika kifungu cha 9(4) na kuweka badala yake maneno "Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya kifungu cha 14(1).

**10.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 14(1) kwa kufuta aya (b) na kuweka badala yake aya (b) mpya kama ifuatavyo:

"(b) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na fedha;"

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta maneno "Waziri wa Fedha" yanayoonekana katika kifungu cha 15 na kuweka badala yake maneno "Waziri anayehusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**12.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 20 kwa kufuta maneno "Tume ya Mipango Zanzibar" yanayoonekana baina ya maneno "Mfuko wa Maendeleo ya Miradi ndani ya" na maneno "ambao unaundwa na" na kuweka badala yake maneno "Wizara inayohusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi".

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**13.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 30 kwa:

(a) kufuta maneno ya pembeni na kuweka badala yake maneno ya pembeni mapya kama ifuatavyo:

"taratibu za miradi iliyoasisiwa na sekta binafsi au sekta ya umma"

(b) kukipa nambari mpya kifungu cha 30 kuwa kifungu cha 30(1); na

(c) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Mamlaka ya Utekelezaji inaweza kuajiri Mshauri au Mtaalamu wa Muda kwa ajili ya kuisaidia Mamlaka ya Utekelezaji au Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kuhusu mambo ya kitaalamu yanayohusiana na Miradi iliyoasisiwa na Sekta Binafsi au Sekta ya Umma."

Marekebisho ya kifungu cha 38.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 38 kwa:

(a) kufuta maneno "miezi miwili" yanayoonekana katika kifungu kidogo cha (5) baina ya maneno "ushauri wa kisheria ndani ya" na maneno "kuhusu Mkataba" na kuweka badala yake maneno "siku ishirini na moja za kalenda."

(b) kufuta maneno "miezi miwili" yanayoonekana katika kifungu kidogo cha (6) baina ya maneno "Wizara ya Fedha ndani ya" na maneno "kama inavyoelezwa na..." na kuweka badala yake maneno "siku ishirini na moja za kalenda."

Marekebisho ya kifungu cha 44.

**15.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 44 kwa:

(a) kuandika upya kifungu kidogo cha (4) kuwa vifungu vidogo vya (4) na (5) kama ifuatavyo:

"(4) Mwekezaji binafsi ataalikwa kushiriki katika utaratibu wowote wa ushindani wa zabuni ulioanzishwa kwa ajili ya kutetea mradi wake aliouasisi.

(5) Mwekezaji binafsi anaweza kubarikiwa mkataba unaohusika na mradi aliouasisi kwa mujibu wa taratibu za ushindani wa zabuni chini ya Sheria hii."

(b) kufuta kifungu kidogo cha (5);

(c) kuongeza vifungu vidogo vipya vya (6), (7), (8), (9) na (10) kama ifuatavyo:

"(6) Mradi ulioasisiwa na Mwekezaji Binafsi utawasilishwa katika Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa ajili ya kuupitia kama umeendana na masharti ya Sheria hii.

(7) Baada ya kuidhinishwa wazo la mradi lililoasisiwa, Mwekezaji Binafsi atatekeleza mradi kwa kuweka dhamana kwa kiwango ambacho kitarejeshwa kisichozidi asilimia tatu za makisio ya gharama za mradi utakaotekelezwa.

(8) Kiwango kilichopaswa kurejeshwa kitachukuliwa kama kiwango kisichopaswa kurejeshwa ikiwa Mwekezaji binafsi atashindwa kutekeleza mradi.

(9) Waziri anayehusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi anaweza kutengeneza Kanuni zinazoelezea taratibu za uwekaji na ulipaji wa dhamana iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (7).

(10) Wazo linalotokana na mradi ulioasisiwa na Mwekezaji Binafsi litapitishwa katika Timu ya Majadiliano ya Serikali kwa ajili ya kutoa mapendekezo kwa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kuidhinishwa".

Kuongeza kifungu kipya cha 44A, 44B na 44C.

**16.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 44A, 44B na 44C kama ifuatavyo:

"Vigezo vya msamaha.

**44A.** Waziri anayehusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi anaweza kuruhusu Mradi ulioasisiwa na Mwekezaji binafsi kutoingia katika taratibu za ushindani wa zabuni endapo atakidhi vigezo vifuatavyo kwamba:

(a) mradi lazima uwe kipaumbele cha Serikali na uendane na Malengo na Mipango Mikakati ya Taifa;

(b) Mwekezaji binafsi asihitaji dhamana ya Serikali au namna yoyote ya msaada wa kifedha kutoka Serikalini;

(c) mradi uoneshe thamani halisi ya kifedha, uwezo na kuhamisha vichocheo hatarishi kwa Mwekezaji binafsi;

(d) mradi uwe na manufaa makubwa ya kijamii na kiuchumi ikijumuisha huduma bora, ajira na kodi;

(e) mwekezaji binafsi atalazimika kugharamia upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii za mradi; na

**(f)** mradi uliopendekezwa na kuwasilishwa uendane na viwango na vigezo vya kimataifa."

"Fursa ya kufanya Mapitio ya mradi uliowasilishwa.

**44B.**-(1) Endapo Mwekezaji binafsi hajatimiza vigezo vilivyoainishwa chini ya kifungu cha 44A cha Sheria hii, ikiwa wazo la mradi ni sahihi, Mwekezaji binafsi anaweza kupewa fursa ya kufanya mapitio ya mradi uliowasilishwa ndani ya siku thelathini tokea tarehe maelekezo yalipotolewa.

(2) Fursa kwa ajili ya kufanya mapitio ya mradi uliowasilishwa haitatolewa zaidi ya mara mbili."

“Timu ya Majadilianao ya Serikali.

**44C**. Kutakuwa na Timu ya Majadiliano ya Serikali ambayo muundo, majukumu na uwezo wake utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni”.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 24 Febuari, 2021.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***